JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

MWONGOZO WA NAMNA SALAMA YA KUWAUNGANISHA NA FAMILIA ZAO WATOTO WAATHIRIKA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

NOVEMBA 2016

United Nations
TANZANIA
Delivering as One

IOM - OIM

EUROPEAN UNION

YALIYOMO

Utangulizi....4

Shukrani....5

Tafsiri Ya Maneno....7

1. Wadau Na Taasisi Zinazohusika Katika Kuunganisha Waathirika Na Jamii Au Familia Zao....8

1.1 Taasisi Zinazohusika Katika Kuunganisha Waathirika Na Jamii/Familia Zao....8

2. Wajibu Na Majukumu Ya Wadau Kutoka Katika Taasisi Zainazohusika Kuunganisha Waathirika Na Familia Zao:....8

2.1 Idara Ya Ustawi Wa Jamii....8

2.2 Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali....9

2.3 Mamlaka Ya Serikali Za Mtaa....9

2.4 Idara Ya Uhamiaji....10

2.5 Jeshi La Polisi Tanzania....10

2.6 Wizara Ya Mambo Ya Nje Na Ushirikiano Wa Afrika Mashariki....10

2.7 Mashirika Ya Kimataifa Na Washirika Wa Maendeleo....10

3. Mambo Ya Kuzingatia Kabla Ya Kumuunganisha Muathirika Na Familia/Jamii Yake....11

3.1 Tathmini Binafsi Ya Maslahi Ya Muathirika Na Kutambua/Kuhakiki Familia Ukizingatia Umri, Jinsi, Ulinzi Na Ulemavu....11

3.2 Zingatia Na Heshimu Haki Za Binadamu Na Utu Wa Muathirika Wakati Wote Wa Mchakato Mzima Wa Kutambua/Kuhakiki Familia....11

3.3 Hakikisha Unapata Ridhaa Kutoka Kwa Muathirika Kabla Ya Kumuunganisha Na Familia/Jamii....11

3.4 Dumisha Usiri Wakati Wote Na Toa Taarifa Pale Tu Inapohitajika....11

3.5 Maadili Ya Utamaduni/ Dini ya Muathirika....12

3.6 Afya Ya Muathirika....12

3.7 Utayari Wa Familia Na Jamii Wa Kumpokea Muathirika....12

3.8 Watoa Huduma Wengine Katika Eneo Husika Ambao Wanaweza Kutoa Msaada Kwa Muathirika Aliyerudishwa....12

4. Kutathmini Hatari Zozote....12

4.1 Hatua Ya 1: Historia Ya Muathirika Wa Usafirishaji Haramu Wa Binadamu....13

4.2 Hatua Ya 2: Kutafiti Taarifa Ya Ziada....13

4.3 Hatua Ya 3: Tengenenza Mazingira Salama....14

4.4 Mazingira Ambayo Huchangia Muathirika Kutounganishwa Na Familia:....14

5. Hatua Za Kufuatwa Wakati Wa Kumuunganisha Muathirika Wa Usafirishaji Haramu Wa Binadamu Na Familia Yake....15

5.1 Hatua Ya Kwanza: Tambua Au Chunguza Kama Kuna Uwezekano Wa Kumuunganisha Muathirika Na Familia Au Jamii Yake....15

5.2 Hatua Ya Pili: Mchakato Wa Maandalizi....16

5.3 Hatua Ya Tatu: Kuunganishwa Na Familia/Jamii....17

5.4 Hatua Ya Nne: Huduma Baada Ya Kuunganishwa Na Familia/Jamii....17

5.4.1 Masuala Mahsusi Ya Kufuatilia Baada Ya Muathirika Kuunganishwa Na Familia/Jamii....18

5.4.2 Ufuatiliaji Na Huduma Baada Ya Kuunganishwa Na Familia/Jamii.....18
Kiambatanisho Cha 1: Njia Za Rufaa Katika Kuwaunganisha
Ya Kukusanya Taarifa Binafsi.....20
Kiambatanisho Cha 2: Tamko La Kurudi Kwa Hiari Na Ruhusa Ya
Kukusanya Taarifa Binafsi 21
Kiambatanisho Cha 3: Fomu Ya Utambuzi Wa Familia (Eneo) Na
Tathmini Ya Familia (Kijamii Na Kiuchumi) Anayotoka Muathirika.....22
Kiambatanisho Cha 4: Orodha Ya Tathmini Ya Hatari.....29
Kiambatanisho Cha 5: Fomu Ya Ruhusa Ya Kuondoka Katika Makazi.....30
Kiambatanisho Cha 6: Orodha Ya Nyenzo Zilizotumika.....32

UTANGULIZI

Usafirishaji haramu wa watoto ni tatizo linalokua Tanzania . Kila mwaka watoto husafirishwa ndani na nje ya mipaka ya nchi. Watoto wanaosafishwa kiharamu wanakumbana na matatizo mengi ikiwemo kulazimishwa kufanya kazi katika mazingira hatarishi, kuuzwa kwa ajili ya kufanyishwa kazi za majumbani, ukahaba au katika picha za ngono. Ongezeko hili la usafirishaji haramu wa watoto limeifanya serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuanza kulitafakari suala hili na kuchukua hatua. Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kupambana na wimbi hili la usafirishaji haramu wa watoto na kuwasaidia watoto walioathirika na usafirishaji haramu wa binadamu. Hatua zilizochukuliwa na serikali ni pamoja na kutunga Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya Tanzania mwaka 2008 , kuunda Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu pamoja na Sekretariti yake mwaka 2011. Lengo la kamati hii ni kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu (2015-2017) na utengenezaji wa kanuni za kutekeleza sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu .

Juhudi hizi zimepokelewa vizuri na wadau wa mashirika yasiyo ya kiserikali wanaotoa huduma za malazi, ushauri nasiha, mafunzo ya ufundi na kuwaunganisha na familia zao waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Pamoja na n kuwepo miongozo ya namna ya kuwalinda na kuwapatia huduma waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hakukua na mwongozo uliokubalika na watoa huduma wa namna ya kuwaunganisha waathirika na familia zao. Kukosekana kwa mwongozo kumefanya watoa huduma kufuata miongozo ya mashirika yao pale wanapounganisha waathirika na familia zao. Hivyo basi kuunganisha watoto walioathirika na usafirishaji haramu wa binadamu hufanyika bila kufuata utaratibu maalumu wala kuzingatia misingi ya haki za binadamu jambo ambalo huwaathiri watoto. Hali hii imelazimisha kutengenezwa kwa mwongozo huu wa namna ya kuwaunganisha watoto na familia zao.

Waathirika wanaweza kuunganishwa kwa namna salama na familia zao pale ambapo wadau mbalimbali wanaohusika wanafahamu mchakato mzima na vigezo vinavyohitajika kufanikisha mchakato huo salama. Lengo kuu la mwongozo huu ni kuwapatia watoa huduma mbalimbali kama vile polisi, maafisa ustawi wa jamii, wafanyakazi wa makao ya watoto, watoa huduma za afya na serikali za mitaa utaratibu na namna salama ya kuwaunganisha watoto na familia zao.

Inategemewa kwamba, mwongozo huu utatoa ueelewa na kuchanganua mchakato gani ufuatwe ili kuunganisha kwa namna salama waathirika na familia zao . Inatarajiwa kwamba wadau mbalimbali wanaohusika na kuunganisha waathirika na familia zao watafuata utaratibu huu ili kukuza mahusiano mazuri katika kazi, njia na utaratibu wa rufaa na hatimaye kutimiza lengo la kuunganisha waathirika na familia zao kwa haraka na kwa ufanisi.

SHUKRANI

Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inawashukuru wale wote walioshiriki katika kuandaa mwongozo huu wa kuwaunganisha watoto walioathirika na usafirishaji haramu wa binadamuna familia zao.

Tunashukuru michango ya wadau mbalimbali walioshiriki wakiwemo Secretariati ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Idara ya Ustawi wa Jamii, Wizara ya Kazi na Ajira, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Shirika la Kuwalinda na Kuwafikia Watoto, Shirika la Kitaifa la Msaada wa Sheria (NOLA), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania, Daughters of Mary Immaculate, Jeshi la Polisi Tanzania, baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Jukwaa la Haki za Watoto Tanzania, Wotesawa Young Domestic Workers Organization, C-SEMA , Watoto Wetu Tanzania na Faraja Vocational Training Centre.

Natoa shukrani kwa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia masuala ya Wahamaji (IOM) Tanzania kwa kutupatia msaada wa kiufundi na kifedha kupitia Timu yake ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu walioandaa rasimu ya kwanza ya mwongozo huu na kuwezesha majadiliano na wadau.

Mwisho kabisa mwongozo huu usingeweza kuandaliwa bila hisani ya Umoja wa Ulaya waliofadhili mradi wa ***"Kusaidia Uanzishwaji wa njia za Ulinzi, Msaada na Taratibu za Rufaa kwa Watoto Waathirika wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu"*** unaoratibiwa na IOM Tanzania.

Dr. Mpoki M. Ulisubisya,
Katibu Mkuu ,
Wizara ya Afya ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto

Mwongozo wa namna salama ya kumuunganisha na familia yake mtoto muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu nchini Tanzania

UTANGULIZI

PALE AMBAPO serikali inatambua sababu za kijamii, kiuchumi na sababu zingine zinazowafanya watu kuhama kutoka katika makazi yao na pia zinawafanya kuwa katika hali hatarishi ya kuathirika na usafirishaji haramu wa binadamu;
NA KWA KUWA tendo hili hufanyika kwa usiri mkubwa inafanya vigumu kutambua wale ambao wameathirika ili kuwapatia msaada muhimu;

KWA KUTAMBUA kuwa baadhi ya taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuja na mipango ya kuwasaidia watoto waliothirika na usafirishaji haramu wa binadamu na kuwaunganisha na familia zao, Idara ya Ustawi wa Jamiii ambayo ndio yenye mamlaka chini ya Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya Tanzania mwaka 2008 ya kuokoa, kulinda na kutoa huduma kwa waathirika imeona mapungufu mengi katika namna amabyo huduma hizi zinatolewa wa waathirika:
KWA KUFAHAMU haja ya kuimarisha mfumo wa ulinzi na utoaji msaada kwa watoto walioathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;

NA KUTHIBITISHA KWAMBA familia ndio mahali sahihi kwa ajili ya makuzi na maendeleo ya mtoto;

NA KUFAHAMU kuwa zipo sababu katika maisha zinazomfanya mtoto kutoka katika familia na kuchagua kuunganishwa na jamii badala ya familia yake, basi ustawi bora au maslahi ya mtoto ndio itakua kigezo cha kuamua mtoto akae na nani;
KWA DHAMIRA ya kuhakikisha kwamba mtoto aliyeathirika na bishara haramu ya binadamu anaunganishwa kwa namna salama na familia yake na kurudi katika jamii huku hatari ya kusafirishwa tena ikiwa imepungua; TUMEAMUA kwa kupitia mwongozo huu kutoa mfumo wa kitaifa wa jinsi ya kuwaunganisha na familia zao watoto walioathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu . Mwongozo huu utaimarisha uratibu wa watoa huduma mbalimbali wanaomsaidia mtoto kuungana na familia yake na kuwezesha kuungana na familia kwa ufanisi na kwa njia ya kudumu.

TAFSIRI YA MANENO [1]

Mtoto : Ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18

Usafirishajii haramu wa watoto: ni kitendo cha kusaili, kusafirisha, kuhamisha, kuhifadhi au kupokea

mtoto kwa lengo la unyonyaji bila kujali njia zilizotumika (nguvu au udanganyifu, aidha ndani au nje ya nchi).

Muathirika wa usafirishaji haramu wa watoto: Mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 (Itifaki ya Palermo; Ibara ya 3)

Kuhakiki Familia : Ni kitendo cha kufuatilia ili kutambua ilipo familia ama ndugu wa muathirika wa

usafirishaji haramu wa watoto katika mchakato wa kumuunganisha mtoto na familia yake.

Jamii ya Wenyeji : Hii ni jamiii ama familia ambayo iko tayari kumpokea, kumuhudumia na kumfanya aishi maisha ya kawaida mtoto ambaye ni muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu .

Uchambuzi wa Hatari : Huu ni utaratibu wa kufafanua na kuchambua hatari dhidi ya waathirika wa usafirishaji haramu wa watoto katika mchakato wa kuungana na familia.

Kunganisha na familia kwa namna salama: Ni kitendo cha kuunganisha waathirika na familia/ jamii zao au nchi za awali kwa kuzingatia utu.

Kuunganisha na familia/jamii kwa namna endelevu: Ni kitendo cha mtoto muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kurudi kabisa katika familia/jamii yake na kuishi maisha ya kawaida.

[1] Tafsiri hizi za maneno zilijadiliwa na kukubalika katika mkutano wa kuandaa mwongozo huu

1. WADAU NA TAASISI ZINAZOHUSIKA KATIKA KUUNGANISHA WAATHIRIKA NA JAMII AU FAMILIA ZAO

Wafuatao ni wadau wanaohusika katika kuunganisha waathirika na familia zao:
Jeshi la Polisi, maafisa wa afya, Maafisa wa Ustawi wa Jamii , Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, wanasheria, madaktari, maafisa uhamiaji, Wajumbe wa Kamati ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Sekretariati yake, jamii na serikali za mitaa (katika ngazi ya kijiji/mtaa/kata na wilaya).

1.1 TAASISI ZINAZOHUSIKA KATIKA KUUNGANISHA WAATHIRIKA NA JAMII/FAMILIA ZAO

Zifuatazo ni taasisi zinazohusika katika kuunganisha waathirika na familia zao:
Idara ya Ustawi wa Jamii, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Wizara ya Mambo ya Ndani: Kamati ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Sekretariati yake, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Polisi Tanzania, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo.

2. WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU KUTOKA KATIKA TAASISI ZAINAZOHUSIKA KUUNGANISHA WAATHIRIKA NA FAMILIA ZAO:

2.1 IDARA YA USTAWI WA JAMII

Idara ya Ustawi wa Jamii chini ya Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya Tanzania ya mwaka 2008 imepewa mamlaka ya kuokoa, kutunza, kutoa huduma na ushauri nasiha kwa waathirika. Kwa kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii, idara ina jukumu la:

i. Kutoa ushauri nasihi kwa waathirika kama watakavyopokea rufaa kutoka kwa Vituo vya Kulinda na Kusaidia Waathirika wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu, lengo ni kuwasaidia waathrika kabla ya kuunganisha na familia/jamii zao;

ii. Kushirikiana na Serikali ya Mitaa kufuatilia na kutathimini familia za waathirika;

iii. Kuratibu na Jeshi la Polisi katika wilaya na vijiji husika ili kupata ulinzi wakati wa zoezi la kuunganisha waathirika na familia/jamiii zao; na

iv. Kutoa ushauri nasihi kwa familia za waathirika .

2.2 MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

Mashirika yasiyo ya kiserikali yana jukumu muhimu katika kutoa malazi kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hivyo kuchangia juhudi za serikali katika kulinda na kusaidia waathirika . Kwa kushirikiana na serikali mashirika yasiyo ya kiserikali yana wajibu wa:

i. Kutoa elimu ya ufundi na mafunzo kwa waathirika katika vituo vyao vya Ulinzi na Msaada kwa Waathirika wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu ili waweze kujitegemea mara baada ya kuunganishiswa na familia zao;

ii. Kutembelea makazi ya waathirika ili kutathmini hali ya eneo na ni kwa namna gani ujuzi alioupata kutokana na mafunzo katika kituo hicho vinaweza kumsaidia muathirika kujitegemea baada ya kuungana na familia;

iii. Kununua vifaa vya kuanzia kazi kwa ajili ya kuwasaidia waathirika kufanya shughuli za uzalishaji na kujipatia kipato na kuishi maisha ya kujitegemea mara baada ya kuunga na familia zao;

iv. Kuwasiliana na waajiri mbalimbali ili kupata ajira kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu baada ya kuwaunganisha na familia/jamii zao;

v. Kuratibu na serikali ya mtaa na Afisa wa Ustawi wa Jamii ili kupata nyaraka muhimu kabla ya kuunganisha waathirika na familia zao;

vi. Kusindikiza waathirika wakati wa kuuwaunganisha na familia zao na inapolazimika kuwasiliana na watekelezaji sheria ili kupata kusindikizwa na polisi;

vii. Kutoa ushauri nasihi kwa familia ya muathirika;

viii. Kufanya ziara ya mara kwa mara ili kufuatilia na kutathmini hali ya muathirika baada ya kuungana na familia.

2.3 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA

Mamlaka ya Serikali za Mtaa ni mdau muhimu katika kusaidia waathirika kuungana na familia zao. Mamlaka ya Serikali za Mtaa inahusisha Wakurugenzi wa Wilaya, Watendaji Kata, Watendaji Mtaa na Kijiji. Wana jukumu la :

i. Kusaidia kutafuta familia ya muathirika na kutathimini hali ya familia katika ngazi ya kijijiji/kata na mtaa;

ii. Kushirikiana na vyombo vya sheria kuhakikisha kwamba muathirika anarudi salama ;

iii. Kuandaa jamii kupokea waathirika na kushiriki katika kutambua na kukabiliana na mahitaji muhimu ya waathirika wanaorejea ;

iv. Kuwaunganisha waathirika na mipangoiliyopo katika serikali za mtaa;

vi. Kutoa nyaraka muhimu kwa ajili ya kuwarudisha waathirika katika jamii zao;

vii. Kusaidia ufuatiliaji na tathmini ya familia ya muathirika baada ya kuungana nayo;

v. Kutoa ushauri nasihi kwa familia ya muathirika na kukuza uelewa wa hatari ya usafirisha haramu wa binadamu.

2.4 IDARA YA UHAMIAJI

Idara ya Uhamiaji ina jukumu kubwa kuunganisha na kurejesha muathirika aliyepelekwa njei ya mipaka ya nchi. Katika tukio ambapo kurejea nchini inaonekana kuwa ndio njia mbadala ilio sahihi basi idara ya uhamiaji ina jukumu:

i. Kuwasiliana na mamlaka ya uhamiaji ya nchi ya asili anayotoka muathirika ili kuwezesha mchakato wa kurejea;

ii. Kutoa nyaraka za kusafiria ili kumuwezesha muathirika kutoka nje ya Tanzania .

2.5 JESHI LA POLISI TANZANIA

Jeshi la Polisi Tanzania lina jukumu la kumsaidia muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kuungana na familia yake. Hivyo basi Jeshi la Polisi lihusishwe hata kama inaonekana kuwa hakuna hali ya kukosekana kwa usalama kwa muathirika. Jukumu la Jeshi la Polisi ni:

i. Kuhakikisha usalama wa muathirika wakati wa kusindikizwa kuungana na jamii/ familia; na

ii. Kutoa nyaraka muhimu kabla ya muathirika kuungana na familia/ jamii.

2.6 WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kushirikiana na balozi za nchi ambayo muathirika yupo ili kuweza kumuunganisha na familia yake.

2.7 MASHIRIKA YA KIMATAFA NA WASHIRIKA WA MAENDELEO

Mashirika ya kimataifa yana jukumu katika kuunganisha waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na familia zao. Majukumu hayo ni :

i. Kutoa jukwaa kwa ajili ya ushirikiano kati ya mashirika mbalimbali na asasi za kiraia;

ii. Kutoa msaada wa moja kwa moja katika kumuunganisha muathirika na familia ama na jamii yake katika nchi yake, au kuunganisha na nchi nyingine ikiwa hataweza kurejea katika nchi yake ya awali. Jukumu hili, haliondolei serikali aliyokutwa muathirika jukumu lake la kuwapa msaada waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu; na

iii. Kutoa msaada na ulinzi katka kusindikiza waathirika wanaorudi nyumbani.

3. MAMBO YA KUZINGATIA KABLA YA KUMUUNGANISHA MUATHIRIKA NA FAMILIA/JAMII YAKE

3.1 TATHMINI BINAFSI YA MASLAHI YA MUATHIRIKA NA KUTAMBUA/KUHAKIKI FAMILIA UKIZINGATIA UMRI, JINSI, ULINZI NA ULEMAVU

i. Hakikisha tathmini binafsi ya maslahi ya watoto waathirika inaanza mara baada tu ya utambuzi na inaendelea mpaka pale suluhisho la kudumu litakapopatikana na kutekelezwa; na
ii. Mtoto apewe taarifa kuhusu jitahada zinazofanyika za kuitambua familia yake na kama kuna hatua yoyote iliyofikiwa.

3.2 ZINGATIA NA HESHIMU HAKI ZA BINADAMU NA UTU WA MUATHIRIKA WAKATI WOTE WA MCHAKATO MZIMA WA KUTAMBUA/KUHAKIKI FAMILIA

i. Hakikisha waathirika wote wanapatiwa haki sawa ya ulinzi bila kujali jinsi, umri, kabila, jamii, ulemavu, utaifa au hadhi ya ukazi/uhamiaji;
ii. Chukua hatua stahiki wakati ukizingatia misingi ya ulinzi na heshima kwa haki za watoto;
iii. Epuka aina yoyote ya ubaguzi dhidi ya mtoto aliyeathirika; na
iv. Hakikisha uhusishwaji wa mtoto katika masuala yoyote ya uhalifu hayaathiri haki yake ya kupatiwa ulinzi maalum.

3.3 HAKIKISHA UNAPATA RIDHAA KUTOKA KWA MUATHIRIKA KABLA YA KU-MUUNGANISHA NA FAMILIA/JAMII

i. Pata ridhaa ya muathirika ya kutamkwa kwa mdomo na ya maandishi kabla ya kumuunganisha na familia/jamii; na
ii. Kama muathirika hajui kusoma au/na kuandika, afisa ustawi wa jamii au mfanyakazi wa kituo amsaidie kujaza fomu kwa niaba yake.

3.4 DUMISHA USIRI WAKATI WOTE NA TOA TAARIFA PALE TU INAPOHITAJIKA

i. Chukua hatua stahiki kulinda faragha na utambulisho wa mtoto aliyeathirika ili kuweza kuhakikisha ulinzi na usalama wa muathirika na familia yake;
ii. Jina, anuani na taarifa zingine zozote ambazo zinaweza pelekea utambuzi wa mtoto aliyeathirika au familia yake visiwekwe wazi kwa umma au vyombo vya habari, isipokuwa pale ambapo taarifa zinahitajika kwa ajili ya kusaidia kuitambua familia au vinginevyo endelea kulinda maslahi ya mtoto;
iii. Usitoe tarifa zozote za mtoto aliyeathirika ambazo zinaweza hatarisha maisha ya mtoto au familia yake;
iv. Fungua jalada na kuweka taarifa za muathirika katika sehemu salama, na
v. Dumisha usiri wa taarifa za muathirika wakati wote.

3.5 MAADILI YA UTAMADUNI/DINI YA MUATHIRIKA

i. Afisa ustawi wa jamii mwenye jukumu la kuitambua familia ya muathirika na kumsindikiza, ni lazima ahakikishe kwamba anaelewa tamaduni, dini, mila, desturi na kanuni ambazo zitazingatiwa mara baada tu ya kufika nyumbani kwa muathirika na muathirika ajulishwe taratibu hizo.

3.6 AFYA YA MUATHIRIKA

i. Kabla ya kumuunganisha muathirika na jamii/familia yake, inabidi muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu apelekwe kwenye kituo cha afya kwa ajili ya uchunguzi wa kina ili kubaini hali ya kiafya ya muathirika na kama anaweza kusafiri. Muathirika ataruhusiwa kuondoka kwenye kituo pale tu atakapokuwa amechunguzwa afya yake na kuonekana mzima; na

ii. Wafanyakazi wa vituo vya afya wanatakiwa kutoa maagizo ya kiafya ya ufuatiliaji zaidi kwa wale waathirika ambao wanahitaji rufaa ya ziada kwa vituo vingine vya afya mara baada ya kuunganishwa na familia/jamii zao kwa mfano waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI watakaohitaji huduma za dawa au huduma ya afya ya kisaikolojia au akili.

3.7 UTAYARI WA FAMILIA NA JAMII WA KUMPOKEA MUATHIRIKA

i. Tathmini utayari wa familia na jamii wa kumkubali na kumpokea muathirika aliyeokolewa. Hii itasaidia kuweza kuamua au kujua mafanikio ya kumuunganisha muathirika na jamii/familia yake.

3.8 WATOA HUDUMA WENGINE KATIKA ENEO HUSIKA AMBAO WANAWEZA KUTOA MSAADA KWA MUATHIRIKA ALIYERUDISHWA

i. Shirikiana na watoa huduma wengine katika eneo hilo ambao wanaweza kumsaidia muathirika aliyeunganishwa na familia/jamii yake;

ii. Fanya kazi na waelimishaji, afisa ustawi wa jamii, na watoa huduma zingine za afya na za kijamii walioko kwenye jamii ili kujenga mtandao imara kwa ajili ya kumsaidia mtoto aliyerudishwa;

iii. Wasiliana na viongozi wa misikiti, mahekalu, makanisa na vituo vingine vya dini ili kuweza kutoa msaada na muongozo wa hisia na imani kwa watoto na familia zao; na

iv. Wahusishe wajumbe wa jamii waweze kutengeneza miradi mahsusi ya kuwasaidia waliounganishwa na familia/jamii zao.

4. KUTATHMINI HATARI ZOZOTE

Fikiria hatari katika ngazi mbili wakati wa kutathmini hatari ili kuona kama kuna uwezekano wa kumuunganisha muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na familia/jamii yake:

i. Hatari halisi ambazo zinamuathiri mtu moja kwa moja na zina uhusiano na kuunganishwa kwa muathirika na familia/jamii yake; na

ii. Hatari zisizo za moja kwa moja katika ngazi ya jamii ambazo zinaweza kupelekea kubaguliwa au kunyanyapaliwa kwa mtu aliyeathirika na usafirishaji haramu wa binadamu.

Hatari hizi zinaweza zisionekane kuwa na uzito katika hali ya kawaida lakini inabidi zitiliwe mkazo hapo

baadae, sababu zinaweza kuchangia kumrejesha muathirika katika hali yake ya awali.
Hatua tatu zifuatazo ni muhimu katika kutathmini hatari kabla ya kumuunganisha muathirka na familia/ jamii yake katika hali salama:

4.1 HATUA YA 1: HISTORIA YA MUATHIRIKA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

i. Hatari kulingana na historia ya mtu: Tathmini familia

ii Hali ya uchumi ya familia iko vipi? Ni mtu gani wa kuaminika kwa muathirika? Je , familia yenyewe iko katika hali ya hatari? Kuna madeni yoyote ambayo familia inayo ama muathirika anayo dhidi ya familia yake? Ni jinsi gani familia imeipokea hali hiyo ya usafirishji haramu wa binadamu?

iii. Hatari zinazosababishwa na mchakato mzima wa usafirishaji haramu wa binadamu:

iv Makundi yaliyohusika na uhalifu: Nani anahusika? Kuna watu gani waliopo kwenye jamii ambayo unadhamiria kumuunganisha muathirika? Kuna uwezekano kiasi gani kwamba wahusika watalipa kisasi baada ya muathirika kurejeshwa? Kundi la wahusika wa uhalifu liko vipi, wahusika wana nguvu gani ya ushawishi?

v. Chunguza na fanya uchambuzi wa familia na marafiki katika jamii:

vi. Marafiki na familia wanaweza kupatikana wapi? Wao wenyewe wako katika hatari au ni kwa kiasi gani aliyesafirishwa yuko kwenye hatari ya kupatikana na wasafirishaji kama ataendelea kuishi na familia? Familia imehama? Je, familia yenyewe inahusika na usafirishaji haramu wa binadamu?

vii. Hatari ya kunyanyapaliwa kwenye jamii: Uchambuzi wa hali halisi ya jamii aliyotoka muathirika; Ni kwa kiasi gani inawezekana kumuunganisha muathirika na familia/jamii yake? Ni kwa kiasi gani inawezekana muathirika kutengwa kutokana na hali yake ya usafirishwaji (amefanya kazi za ngono/ umalaya)?

viii. Uchambuzi wa mazingira atakayoishi muathirika katika jamii yake: Kuna nafasi kiasi gani kwa muathirika kuweza kushirikiana na watu katika jamii yake kulingana na historia yake?

4.2 HATUA YA 2: KUTAFITI TAARIFA YA ZIADA

Kusanya taarifa zaidi kuhusu jamii anayotoka muathirika mbali ya yale ambayo yamekwisha kukusanywa kupitia mahojiano na muathirika. Tumia vyanzo vya kuaminika vya kukupatia taarifa kama vile mashirika yasiyo ya kiserikali au wasiliana na kushirikiana na watumishi wa serikali na:

i. Tafiti mtu wa kuweza kuwasiliana naye: Ni aina gani ya watumishi wa serikali unaweza kuwasiliana nao? Ni aina gani ya taarifa unaweza kuipokea kutoka kwa watumishi wa serikali bila kumuweka muathirika katika hali ya hatari;

ii. Taarifa kutoka kwenye mashirika maalum yasiyo ya kiserikali: Ni kwa jinsi gani wataalamu kutoka kwenye jamii wanapima hali halisi ya ulinzi na usalama ikilinganishwa na uwezekano wa kumuunganisha muathirika na familia/jamii yake? Ni aina gani ya msaada wa tiba ya kimwili na kisaikolojia inayotolewa?

iii. Tafuta taarifa zaidi kutoka mashirika ya kimataifa.

Lengo la kutekeleza hatua hizo mbili muhimu kabla ya kuendelea na hatua ya tatu ni ili kujua kama kuna uwezekano wowote wa hatari pale ambapo muathirika atarejeshwa.

4.3 HATUA YA 3: TENGENENZA MAZINGIRA SALAMA

- ❖ Tengeneza ushirikiano wenye ufanisi kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yanatathmini hatari hizo na watendaji wa serikali; na
- ❖ Kabla ya kuanza kumuunganisha muathirika na familia/jamii yake, tengeneza mpango wa usalama ukizingatia historia ya muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Zingatia yafuatayo:
- ➢ Je kuna haja ya kutoa ushauri wa kumuunganisha muathirika na familia/jamii ingine?
- ➢ Kuna uhitaji wa kusindikizwa na polisi?
- ➢ Ni aina gani ya taarifa isiwekwe hadharani kwa umma kwa sababu ya hatari ya kunyanyapaliwa?
- ➢ Kama kuunnganishwa na familia/jamii yake hakupendekezwi, kuna njia gani mbadala za kuunganishwa na jamii zingine ambazo zimewekwa/zimeanzishwa?
- ➢ Kuna ujuzi au sifa gani ambazo muathirika amezipokea kutoka kwenye vituo vya kulinda na kutoa msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ambazo zitafanya mchakato mzima wa kuunganishwa na familia uwe na uwezekano wa kuwa wa kudumu/endelevu?
- ➢ Je, Uponyaji wenye ufanisi wa kimwili na kiakili utahakikishwa? Ni kitu gani ambacho kinatolewa katika jamii?
- ➢ Kama ikitokea wasafirishaji wako kwenye jamii husika, ni kwa jinsi gani wanaweza kuepukwa?
- ➢ Ni kwa kiasi gani usalama unaweza kuhakikishwa?

Kama kuunganishwa kwa namna salama na familia/jamii/kurudishwa (kwa wale waathirika kutoka nchi zingine) haiwezi kuhakikishwa kulingana na uchambuzi wa hatua za awali, lakini muathirika bado anataka kuondoka kwenye kituo sababu ya sonona, Je, kuna uwezekano wa kumuweka na familia au jamii nyingine au kuhamishwa katika nchi ya tatu? Ni nchi gani anaona zinafaa kama njia mbadala? Baadae, chambua mambo yote yaliyoainishwa.

4.4 MAZINGIRA AMBAYO HUCHANGIA MUATHIRIKA KUTOUNGANISHWA NA FAMILIA:

i. Muathirika hataki kurudi nyumbani (Maamuzi ya kurudi yanategemea ukosefu wa malengo ya maisha kwa familia anayokwenda, jamii au nchi);

ii. Kuna uwezekano mkubwa wa hatari kutokana na ushahidi uliotolewa kwenye kesi ya jinai, wasafirishaji wanasubiri kurejeshwa kwa muathirika ili walipe kisasi;

iii. Mtandao wa uhalifu wa msafirishaji unaweza kuwashawishi polisi au watendaji wengine wa serikali wa nchi ya asili; na

iv. Hatari kubwa sababu ya familia na jamii ya karibu kujihusisha na mchakato mzima wa usafirishaji haramu wa binadamu.

Katika mambo yote yaliyotajwa hapo juu, uwezekano wa kurejeshwa katika hali ya uathirika au kuwa muathirika wa mambo mengine ambayo yanakiuka haki za binadamu ni mkubwa sana.

5. HATUA ZA KUFUATWA WAKATI WA KUMUUNGANISHA MUATHIRIKA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU NA FAMILIA YAKE

Kumuunganisha muathirika na familia au jamii yake sio kitendo cha mara moja bali ni mchakato unaohusisha hatua na wadau mbalimbali. Inashauriwa kuanza maandalizi au mchakato wa kumuunganisha muathirika na familia au jamii yake haraka iwezekanavyo, haswa mara tu baada ya kumtambua mtoto aliyeathirika na usafirishaji haramu wa binadamu.

5.1 HATUA YA KWANZA: TAMBUA AU CHUNGUZA KAMA KUNA UWEZEKANO WA KUMUUNGANISHA MUATHIRIKA NA FAMILIA AU JAMII YAKE

- Kwa kupitia utoaji wa ushauri nasihi/mahojiano/mikutano na muathirika, chunguza na kuelewa historia ya familia anayotoka muathirika; kama kuna vitendo vya ukatili; hisia/tabia; majukumu mbalimbali kwenye familia na mahusiano kati ya wanafamilia na msafirishaji na mnyonyaji. Lazima uelewa maisha ya mtoto yakoje ndani ya familia hiyo.
- Kwa kawaida maandalizi au mchakato huu uchukue kati ya miezi miwili au mitatu. Utambue ya kwamba mara nyingi miezi miwili mpaka mitatu haitoshi. Kwa baadhi ya kesi muda unaweza kuwa hata chini ya miezi miwili. Hii hutokea pale ambapo familia imetambuliwa kwamba haikuhusika na mchakato wowote wa usafirishaji haramu wa binadamu na mazingira ya familia ni chanya au yanaridhisha. Katika hali hii ni lazima utambue chanzo cha mtoto kusafirishwa.

Mtoto atarejeshwa pale ambapo tu hali /mazingira yafuatayo ya kuunganishwa na familia au jamii yanawezekana:

i. Mtoto yuko tayari kuunganishwa na wanafamilia, ndugu wengine au walezi/watoa huduma.

ii. Mazingira ya familia ya awali yanaruhusu mtoto kurudi. Hii ina maana:
   - Wazazi au walezi wa mtoto wametambuliwa, wamepewa taarifa na wamekubali kumpokea au kumchukua mtoto;
   - Wazazi au walezi wamepewa taarifa kuhusu kurudi kwa mtoto na wametambua umuhimu wa kumuonyesha mapenzi na kumpatia matunzo ya hali ya juu (Hakuna ukatili wa kimwili au kiakili) kwa mtoto, kipaumbele ikiwa ni furaha ya moto;
   - Wazazi au walezi wana uwezo na nia ya kumpatia lishe bora, elimu stahiki, malazi, matunzo ya afya na mahitaji mengine muhimu. Pia jamii inatoa ushirikiano kwa familia na inahakikisha kwamba mtoto anapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa familia.

iii. Wanafamilia au watoa huduma/walezi wametambuliwa na wamepewa taarifa pale ambapo muathirika hawezi kurudi kwenye familia yake ya awali (yaani pale ambapo bado kuna matatizo ya ulevi, ukatili, unyanyasaji au umasikini wa kupindukia).

iv. Pale ambapo muathirika anaweza kujitegemea na amejengewa uwezo/amewezeshwa ukilinganisha na kipindi kabla ya kuondoka kijijini/nyumbani. Hii ina maana muathirika amemaliza masomo yake na amepata ujuzi mpya kwa kupitia mafunzo ya ufundi au/na kapata kazi chini ya udhamini/uangalizi wa shirika linalotoa huduma hizo.

5.2 HATUA YA PILI: MCHAKATO WA MAANDALIZI

Kumuunganisha mtoto na familia au jamii inaweza ikawa kipindi kigumu chenye kuleta mkanganiko kwa wanafamilia mbalimbali, amabao wanaweza kuwa na hisia mbalimbali, hasi na chanya kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba siyo tu familia iko tayari kumpokea mtoto, lakini pia kukubali na kutoa matunzo stahiki kwa mtoto huyo.

Hatua ya maandalizi inahusisha kutambua mahitaji na wasiwasi mwingine alionao muathirika, yaani matakwa yake na upendeleo wake katika kuchagua utaratibu fulani wa kuunganishwa na familia au jamii yake, na pia huduma za kumsaidia au fursa zilizoko ambazo kwa njia moja au nyingine zinaweza kuingiliana au kuathiri uunganishwaji na familia/jamii.

Hatua hii pia inahusisha utafutaji wa familia na kutembelea nyumbani kwa muathirika, vyote vikiwa na lengo la kutathmini uwezekano wa kumuunganisha muathirika na familia/jamii yake au/na kutafuta njia mbadala kwa muathirika. Ni lazima yafuatayo yawe sehemu ya mchakato mzima wa maandalizi:

i. Watoa huduma wawajengee uwezo waathirika ili kupata ujuzi mpya na kuweza kujitegemea au kusimama kwa miguu yao na kutokuwa katika hali hatarishi. Ni lazima wawasiliane na muathirika ili kujua matakwa yake baada ya kuunganishwa na familia/jamii kulingana na ujuzi/mafunzo waliyoyapata.

ii. Ni muhimu kuwa na ushirikiano na uratibu mzuri kati ya watoa huduma kwenye vituo, maafisa ustawi wa jamii, maafisa wa serikali za mitaa na wafanyakazi wa mashirika yasiyo ya kiserikali wakati wa hatua ya maandalizi na kutembelea nyumbani kwa muathirika. Kwenye maeneo ambayso maafisa ustawi wa jamii hawapo, maafisa wa maendeleo ya jamii wanaweza kutumika katika kutoa msaada.

iii. Kwenye maeneo ambayo watoa huduma wa vituo au maafisa ustawi wa jamii hawawezi kutemebelea familia, ni lazima washirikiane na maafisa wa serikali za mitaa ambao wanaweza kutembelea familia ili kutathmini hali halisi ya familia alafu wakatoa taarifa iwapo mazingira hayo yanafaa kumuunganisha mtoto na familia/jamii au la.

iv. Huduma saidizi na fursa zilizoko kijijini/kwenye jamii ni lazima zitambuliwe mapema iwezekanavyo kabla ya kuunganishwa na familia/jamii. Maafisa ustawi wa jamii na wafanyakazi wa vituo wanatakiwa kuwasiliana na maafisa wanaotembelea familia ili kuweza kutathmini fursa zilizopo kwa ajili ya muathirika kama vile mafunzo ya ufundi, elimu iliyo rasmi, biashara/ujasiriamali na nafasi za kazi.

v. Maafisa wa serikali za mitaa wanatakiwa kuiandaa familia au kijiji/jamii kwa ujumla ili kuweza kumpokea na kumkubali muathirika.

5.3 HATUA YA TATU: KUUNGANISHWA NA FAMILIA/JAMII

Baada ya tathmini kufanyika (kutambua na kutemeblea familia) na imebainika kwamba muathirika anaweza kurudi kwenye jamii au nchi yake, watoa huduma wanatakiwa kutoa taarifa hiyo kwa muathirika na kuanza taratibu za safari ili kumuwezesha muathirika kusafiri salama kuelekea kwenye familia/jamii aliyotoka. Kazi ya kumuunganisha muathirika na familia/jamii yake inaweza ikafanywa na maafisa ustawi wa shirika au na wafanyakazi wa serikali wanaojulikana kama maafisa ustawi wa jamii. Ni muhimu kutambua kwamba watoto wanatakiwa kusindikizwa wakati wote wa kurejeshwa na huduma stahiki itolewe kwa watoto wenye mahitaji maalum, haswa wale wenye ulemavu, matatizo ya akili, wagonjwa au wenye uja uzito.

Maafisa ustawi wa mashirika au maafisa ustawi wa jamii wanatakiwa kufanya matayarisho ya kutosha yafuatayo ya kumrejesha muathirika:

i. Wanatakiwa kuhakikisha kwamba kuna ridhaa ya maandishi ya muathirika.

ii. Ruhusa ya kusafiri inatakiwa ipatikane kutoka kwa kitengo husika cha serikali kama Kitengo cha ustawi wa jamii au Polisi. Muathirika ataruhusiwa kuondoka kwenye kituo au shirika pale tu ambapo atakuwa amepata ruhusa ya maandishi iliyosainiwa.

iii Kwa waathirika ambao sio raia, nyaraka muhimu za kusafiria zichukuliwe kutoka kitengo cha uhamiaji. Pale ambapo msaada wa njiani utahitajika, ni muhimu taarifa itolewe kwa wahusika kabla muathirika hajaanza safari.

iv. Wafanyakazi ambao ni maafisa kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali au maafisa ustawi wa jamii wafanye tathmini kama kuna hali hatarishi za usalama au ulinzi wakati wa safari na inapobidi waombe kusindikizwa na polisi.

v. Mipango mingine ya safari inahusisha usafiri, malazi wakiwa njiani pale inapobidi na manunuzi ya vifaa muhimu (vya shule au biashara).

vi. Baada ya kufika mwisho wa safari, mfanyakazi aliyeambatana na muathirika anatakiwa kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa familia/ndugu/mlezi ya kukubali kumpokea muathirika

vii. Kulingana na mazingira, na kama muda unaruhusu, afisa ustawi wa jamii au mfanyakazi wa kituo, atamsaidia muathirika kuweka mambo ya biashara yake sawa au kumsajili na shule au chuo cha ufundi. Kama hili haliwezekani, wanafamilia wakishirikiana na serikali za mitaa/kijiji wamsaidie muathirika katika kujipanga au kujiweka sawa.

viii. Mfanyakazi wa kituo au afisa ustawi wa jamii aliyeambatana na muathirika akisaidiana na maafisa wa serikali za mitaa, waitishe mkutano na familia/ndugu/mlezi na wanajamii wengine ili kuelezea sababu zilizomfanya muathirika akaondoka na pia kuhamasisha kuhusiana na suala zima la usafirishaji haramu wa bidnadamu.

ix. Mfanyakazi wa kituo au afisa ustawi wa jamii aliyeambatana na muathirika atakusanya taarifa za mawasiliano za watu angalau watatu kutoka kwa wanafamilia, ndugu, marafiki na viongozi katika jamii ili kuweza kuwasiliana nao na kupata habari/taarifa za muathirika.

5.4 HATUA YA NNE: HUDUMA BAADA YA KUUNGANISHWA NA FAMILIA/JAMII

Kuna changamoto nyingi na matatizo ambayo watoto wanakumbana nayo mara baada ya kurejeshwa nyumbani. Matatizo haya mengi na mapana yanawakilisha vipangamizi ambavyo vitamuathiri mtoto pale ambapo hatua stahiki hazitachukuliwa, na yanaweza kusababisha unyanyasaji zaidi na hatimaye kurejeshwa

katika hali ya mwanzo ya usafirishaji. Ni muhimu kwa wadau na mashirika kuendelee kutunza taarifa za mawasiliano za waliounganishwa na familia/jamii zao, hata baada ya muda mrefu wa kurejeshwa, ili kuweza kufuatilia maendeleo yao na kutoa msaada pale ambapo inabidi. Tunza taarifa za mawasiliano za aliyerejeshwa ili kuhakikisha kwamba kurejeshwa huko na kuunganishwa na familia/jamii ni endelevu na kukusaidia pia kuweza kutambua wale waliorejeshwa katika hali ya mwanzo ya usafirishaji.

5.4.1 MASUALA MAHSUSI YA KUFUATILIA BAADA YA MUATHIRIKA KUUNGANISHWA NA FAMILIA/JAMII

Baadhi ya masuala mahususi ambayo yanaweza kufuatiliwa ni kama ifuatavyo:

- Kama mtoto anaonyesha kuridhika na maisha ya familia;
- Kama mtoto anatendewa sawa na watoto wengine kwenye familia;
- Kama mtoto anahudhuria elimu iliyo rasmi au isiyo rasmi;
- Kama mtoto anasiriki kwenye masuala ya jamii;
- Kama angalau mtu mmoja katika familia ana kipato, au anatoa huduma muhimu zakuitosheleza familia;
- Kama hakuna wasiwasi wowote kwenye masuala ya ulinzi.

5.4.2 UFUATILIAJI NA HUDUMA BAADA YA KUUNGANISHWA NA FAMILIA/JAMII

Baadhi ya mambo yanachangia ni kwa kiasi gani mtoto anahitaji kufuatiliwa baada ya kuunganishwa na familia/jamii yake .

Umbali na hali ya eneo ni mambo yanayochangia maamuzi ya mashirika yanayofanya kazi na watoto katika mkoa/wilaya hata nchi za jirani. Inawezekana miundombinu imeharibika au haijitoshelezi, ambayo inaweza kuzuia uwezo wa mashirika kutoa msaada wa kiwango kwa watoto. Pale ambapo wanakumbana na hizi changamoto, ni muhimu kuwasiliana na wadau wengine, ikiwemo kusaidia mifumo ya kijamii ya ulinzi wa watoto kama vile timu za ulinzi wa mtoto.

ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho cha 1: Njia za rufaa katika kuwaunganisha waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na familia zao
Kiambatanisho cha2: Tamko la kurudi kwa hiari na ruhusa ya kukusanya taarifa binafsi
Kiambatanisho cha 3: Fomu ya utambuzi wa familia (eneo) na tathmini ya familia (kijamii kiuchumi) anayotoka muathirika
Kiambatanisho cha 4:Orodha ya tathmini ya hatari
Kiambatanisho cha 5:Fomu ya ruhusa ya kuondoka katika makazi
Kiambatanisho cha 6: Orodha ya nyenzo zilizotumika

KIAMBATANISHO CHA 1: NJIA ZA RUFAA KATIKA KUWAUNGANISHA WAATHIRIKA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU NA FAMILIA ZAO



KIAMBATANISHO CHA 2: TAMKO LA KURUDI KWA HIARI NA RUHUSA YA KUKUSANYA TAARIFA BINAFSI

Angalizo: Tafadhari mruhusu mtu aisome fomu (au hakikisha inaweza kutafsiriwa katika lugha anayoielewa) na uielezee kabla ya kumuomba asaini fomu hii.

Mimi, niliyeweka saini hapo chini, _____, naeleza uamuzi wangu wa hiari kurudi kijijini/mjini/nchini kwangu au kwenda katika nchi ya tatu (ambapo nina haki ya kupewa makazi ya kudumu) ambayo ni _____, kwa kupitia msaada wa ……. (*Taja jina la shirika*). Naelewa kwamba sitaruhusiwa kukaa kwa muda katika nchi yoyote nitakayopitia wakati wa safari yangu. (*kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wa nje wa mipaka ya nchi zao*).

Naelewa kwamba taarifa zangu binafsi na za wategemezi wangu _____ _____ (*taja jina la mtoto/wanafamilia*) ni muhimu katika utolewaji wa msaada huu. Nimefahamishwa kuhusu madhumuni maalumu na ya ziada na hivyo basi ninaruhusu _____ *(taja jina la shirika)* na mtu mwingine yeyote anayeruhusiwa au taasisi inayofanya kazi kwa niaba ya ……. (*Taja jina la shirika*) kukusanya, kutumia na kutoa taarifa binafsi katika fomu hii. Ninaelewa na ninakubali kwamba taarifa hizi binafsi zitapelekwa kwa/ na zitashughulikiwa na _____ (*Jina la mtu wa tatu kwa mfano wafadhili, mashirika husika/taasisi za kiserikali*) ili kufanikisha lengo muhimu.

Hivyobasi, mimi mwenyewe, pamoja na wategemezi wangu, warithi wangu na mali zangu na kubali kutowapa hatia (*taja jina la shirika*) wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja, kwangu, kwa mtoto wangu au kwa familia yangu kuhusiana na idhini hii.

Ninakiri kwamba taarifa niliotoa ni ya kweli na sahihi kwa kadri ya uwezo wangu. Naelewa kwamba kama nikitoa kauli za uongo katika kusaini fomu hii, msaada unaotolewa na …… (*taja jina la shirika*) unaweza ukasitishwa muda wowote.

Imesainiwa tarehe_____ mahali_____: _____

Saini ya muombaji: _____

Saini ya mkalimani (*kama ametumika*): _____

Saini ya mwakilishi wa shirika au mjumbe: _____

[MUHURI WA SHIRIKA]

KIAMBATANISHO CHA 3: FOMU YA UTAMBUZI WA FAMILIA (eneo) NA TATHMINI YA FAMILIA (kijamii na kiuchumi) ANAYOTOKA MUATHIRIKA

Utangulizi:
Kabla ya kuanza tathmini, ambayo itafanyika kwa mahojiano shirikishi na familia, tafadhali wajulishe wahojiwa lengo la tathmini. Lengo ni kukusanya taarifa juu ya hali ya kijamii na kiuchumi ya familia ili kuwa na uwezo wa kutathmini nini inaweza kuwa chaguzi sahihi kwa mtoto katika muda mfupi na kwa muda mrefu. Tathmini ya familia kwa hali yoyote haitofanyika kwa kutumia nguvu ya namna yoyote ile. Baada ya kumaliza kufanya tathmini ya familia na uthibitisho wa wazazi / au walezi wa kisheria juu ya taarifa zilizotolewa, afisa wa ustawi wa jamii / afisa wa shirika lisilo la kiserikali watamfuatilia ipasavyo muathirika aliyeko kwenye kituo cha ulinzi na msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na / au mlezi wa kisheria atahitimisha juu ya uwezekano wa kumunganisha / kumrejesha na jamii muathirika huyo.

Kipengele cha 1: Ridhaa ya utambuzi wa familia na tathmini ya familia anayotoka muathirika
Mimi, nakiri ridhaa yangu kwamba afisa wa shirika lisilo la kiserikali / afisa wa ustawi wa jamii wa serikali atafanya, kwa kuzingatia taarifa zinazotolewa, utambuzi wa familia na tathmini ya familia kwa lengo la kuniunganisha kwa hiari yangu na familia/ jamii/ kurejeshwa/ kutafutiwa makazi mapya katika kesi za kipekee.

Saini ya mwombaji:

Jina:

Saini ya mlezi wa kisheria:

Jina:

Mahali na tarehe:

1.1 Taarifa ya ujumla ya muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu

Jina la muathirika	
Tarehe ya kuzaliwa (siku/mwezi/mwaka)	
Umri	
Jinsia	
Mahali pa kuzaliwa	
Uraia	

Mahali pa Kuishi

[ ] katika kituo cha malazi
[ ] na watu wa familia
[ ] na marafiki
[ ] na familia ya kufikia isiyo ya asili
[ ] mengine
Taja: _____

Mlezi wa Kisheria:

Jina:

Anuani:

Namba ya simu:

Barua pepe:

Ushirikiano
(Tafadhali taja kama kuna ushirikiano katika ngazi ya chini au ngazi ya kitaifa - kwa mfano, afisa ustawi wa jamii ngazi ya chini/kitengo cha ustawi wa jamii ngazi ya kitaifa, taasisi zisizo za kiserikali nk - zilihitajika kutekeleza mahojiano)

[ ] hapana
[ ] za kiserikali
[ ] mengine
Taja: _____

1.2. Taarifa ya ujumla ya eneo la familia

Jina la Mama:	
Jina la Baba:	
Jina la mlezi yeyote:	
Anuani:	
Namba ya simu:	
Namba ya simu ya mkononi:	
Barua pepe:	
Taarifa nyingine yoyote ambayo inawe-za kuwa muhimu katika hatua hii:	

Kipengele cha 2: Tathmini ya familia anayotoka muathirika (Ikamilishwe na shirika lililowajibika kufanya tathmini ya familia)

Uhusiano na mtoto:

1) Babu;
2) Bibi;
3) Mama;
4) Baba;
5) Kaka;
6) Dada;
7) Mjomba;
8) Shangazi;
9) Binamu wa kiume;
10) Binamu wa kike;
11) Ndugu yoyote;
12) Watendaji wa serikali za mitaa;
13) Kiongozi wa jamii;
14) Kiongozi wa dini;
15) mengine, Taja:_____

Muundo wa kaya[2]

1. Tafadhali orodhesha watu wote wa kaya (hata kama hakuwepo wakati wa mahojiano)

Mwaka wa kuzaliwa	Uhusiano[3]	Mlezi Ndio/Hapana	Elimu[4]	Shughuli[5]	Matatizo ya kiafya[6]	Jina la kwanza na Jina la Ukoo

2. Je, wazazi wanaishi pamoja katika kaya moja? [ ] Ndio; [ ] Hapana

   2A) Kama hapana, kwanini?

   [ ] wametengana / wametalakiana

   [ ] amefariki

   [ ] amehama

   [ ] mengine,

   taja: _____

[2]Kaya inaelezwa kuwa ni watu ambao wanaishi chini ya paa moja na kushiriki angalau mlo mmoja wa pamoja kwa siku.

[3]1) Babu; 2) Bibi; 3) Mama; 4) Baba; 5) Kaka; 6) Dada; 7) Mjomba; 8) Shangazi; 9) Binamu wa kiume; 10) Binamu wa kike; 11) Ndugu yoyote; 12) Mamlaka ya mitaa; 13) Kiongozi wa jamii; 14) Kiongozi wa dini 15) mengine, Taja:_____

[4] 1) Hakuna Elimu; 2) Elimu ya Msingi (mwaka wa 1-8 wa shule); 3) Elimu ya sekondari (mwaka wa 9-13 wa shule); 5) Elimu ya ufundi; 5) Elimu ya chuo kikuu; 6) mengine:_____

[5]1) hajaajiriwa; 2)mwanafunzi; 3) mkulima/mvuvi/; 4) muajiriwa wa mara kwa mara 5) muajiriwa (nje ya rekodi); 6) amejiajiri 7)mfanyakazi wa mara kwa mara; 8) mama wa nyumbani; 9) Mengine; taja: _____

[6]1) ulemavu wa kimwili; 2)ugonjwa ; 3) hakuna; 4) mengine:_____

Hali ya maisha, kijamii na kiuchumi katika kaya

3. Tafadhali eleza nani, miongoni mwa waliotajwa hapo juu, ana/wanaingiza kipato kusaidia familia.
4. Kipato cha familia: (Tafadhali rejea kwenye miongozo kwa ajili ya ufafanuzi zaidi juu ya mahitaji ya msingi/mahitaji mengineyo)

   [ ] Ni cha kutosha kukidhi pia mahitaji mengineyo ya familia

   [ ] hukidhi mahitaji ya msingi pekee

   [ ] si cha kutosha kukidhi mahitaji ya msingi ya familia

   [ ] hakuna kipato cha familia

5. Eneo la makazi ya familia:

   [ ] kijiji

   [ ] mji

   [ ] mazingira ya kijijini

   [ ] makazi duni

   [ ] Mengine,

   taja: _____

6. Aina ya makazi ya familia:

   [ ] nyumba ya familia moja

   [ ] nyumba zilizoko kwenye eneo moja

   [ ] Makazi duni

   [ ] mengine,

   taja: _____

7. Tafadhali eleza kwa ufupi hali ya majirani wa eneo hilo:
8. Je, makazi ya familia ni ya kudumu au ya muda?

Taarifa inayohusu kuondoka kwa watoto wasio na usimamizi/uangalizi wa wazazi

9. Kama anayehoji anaona kuwa kuna unawezekano, tafadhali toa maelezo ya mazingira yanayozunguka kuondoka kwa mtoto?

   [ ] kwa sababu za kiuchumi

   [ ] familia haikuweza kufuatilia/kulea mtoto

   [ ] familia/mtoto alikua na ndugu nje ya nchi

   [ ] kwasabau familia yake ilimtia moyo kufanya hivyo

[ ] kwa sababu ya migogoro/matatizo kati ya mtoto na familia

Mengine; taja: _____

10. Ni mara ngapi kumekuwa na mawasiliano na mtoto tangu ameondoka?

[ ] Siku

[ ] Kila wiki

[ ] Kila mwezi

[ ] Mara chache kwa mwaka

[ ] Kamwe

[ ] Mengine, taja: _____

11. Kama mtoto atataka kurudi nyumbani, familia yake itakubali kumpokea kama mmoja wa familia?

[ ] ndio

[ ] sijui

[ ] hapana

[ ] mengine, taja: _____

12. A) Kama hapana, kwanini?

[ ] Kwa sababu za kiuchumi

[ ] Kwa sababu familia imegawanyika /wazazi wamegawanyika

[ ] Familia haiwezi kumtunza

[ ] Familia imewekeza fedha nyingi katika safari yake

[ ] Familia inahitaji fedha zake (fedha kutoka nje)

[ ] Kwa sababu ya migogoro/matatizo kati ya mtoto na familia

Mengine; taja:_____

Maoni mengine yoyote ambayo yanaweza kuwa ya muhimu

Tafadhali wakaribishe waliohojiwa kutoa nyongeza kwa maswali yaliotajwa hapo juu, kama watapendelea.

Kwa niaba ya anayehojiwa:

* Nimefahamishwa kwamba taarifa zilizokusanywa tena wakati wa mahojiano zitatumika kuamua ni njia zipi mbadala ni bora kwa maslahi ya (tafadhali ongeza na jina la mtoto).

* Nimefahamishwa kwamba taarifa zilizokusanywa wakati wa mahojiano zitabaki madhubuti ndani ya shirika (jina hilo) na kutumika tu kwa madhumuni ilivyoelezwa hapo juu.

* Ninathibitisha kwamba taarifa iliotolewa wakati wa mahojiano ni sahihi kwa kadri ya ufahamu wangu

Kwa kutia saini fomu hii, nashuhudia kwamba nilishiriki katika mahojiano kwa uhuru:

Saini ya mzazi/au mlezi halali wa kisheria:

Jina:

Mahali na tarehe:

Kwa niaba ya anayehoji:

Nathibitisha kwamba mshiriki alipewa nafasi ya kuuliza maswali kuhusu mradi huu, na maswali yote yalio-ulizwa na mshiriki yamejibiwa kwa usahihi na kwa kadri ya uwezo wangu.

Nathibitisha kwamba mshiriki hajashurutishwa kutoa idhini yake, na ridhaa/ idhini yake imetolewa kwa uhuru na kwa hiari.

Saini:

Jina:

Mahali na tarehe:

KIAMBATANISHO CHA 4: ORODHA YA TATHMINI YA HATARI

Muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kwa hiari yake anataka kurejeshwa/kuunganishwa na familia yake na amejaza fomu ya ridhaa:	NDIO	HAPANA
Kama ni muhimu: Kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wenye matatizo ya kiafya, kuna msaada kwao kabla ya kundoka kama vile: a. Kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa banadamu wenye matatizo ya kimwili, daktari asaini fomu kwamba afya yake inaruhusu kusafiri b. Kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wenye matatizo ya afya ya akili hakikisha mtu ana uwezo wa kutoa maamuzi madhubuti (tathmini ya kisaikolojia isainiwe)		
Kwa watoto wanaosafirishwa: kabla ya kumrudisha mtoto aliyesafirishwa kiharamu, shirika linalomrudisha ni lazima lithibitishe: a. Kwamba utambuzi wa maslahi ya mtoto umefanyika (na afisa utawi wa jamii, meneja wa kituo na/au mlezi wa kisheria) b. Kwamba utambuzi wa maslahi ya mtoto umethibitisha kuwa kurudishwa kwa mtoto ni kwa manufaa yake c. Shirika linalomrudisha mtoto katika familia/jamii yake linapaswa liyape kipaumbele maoni ya mtoto katika mchakato mzima wa kumuunganisha na familia/jamii. d. Kwamba mlezi wa kisheria wa mtoto amepewa taarifa kuhusu kurejeshwa kwa mtoto		
Uhamisho salama wa mtu aliyesafirishwa umepangwa		
Ulinzi wa taarifa dhidi ya unyanyapaa na matumizi mabaya umehakikishwa		
Kuna uwezekano wa kuwaunganisha katika jamii zao na katika soko la ajira. Kwa watoto waliosafirishwa: kuna uwezekano wa kuwaunganisha (kwa mfano kwenye mfumo wa shule)		
Athari zinazohusiana na mtandao wa wasafirishaj haramu hautishii maisha au afya ya mtu aliyesafirishwa au wapendwa wao.		
Kuna uwezekano mdogo wa magenge ya wahalifu kulipa kisasi dhidi ya watu waliosafirishwa au kuwadhibiti		
Vyombo vya kutekeleza sheria katika jamii ya asili ya muathirika vina uwezo wa kutoa ulinzi madhubuti kwa ajili ya watu waliosafirishwa kiharamu		
Kuna uchunguzi wa kesi ya jinai/ kesi mahakamani ambapo kuna uwezekano wa muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kulipwa fidia		
Kiwango cha serikali za mtaa katika kujitoa kusaidia kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu katika jamii ya asili ni kikubwa		
Kuna njia mbadala katika jamii ya awali za kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wasisafirishwe kiharamu tena		
Rushwa katika nchi na/au jamii ya asili haijaenea na haiongezi hatari kwa kiasi kikubwa		

Angalizo: Endapo jibu lolote la maelezo hapo juu ni “HAPANA” tafadhali elezea mpango wa kupunguza hatari zinazotarajiwa:

Maamuzi ya msimamizi wa kesi kulingana na orodha ya tathmini ya hatari:

Endelea na mchakato wa kumuunganisha na familia

Endelea na mchakato wa kumuunganisha na jamii

Haiwezekani kumuunganisha na familia/jamii. Kama ni shirika lisilo la kiserikali, toa rufaa ya kesi kwa afisa ustawi wa jamii wa wilaya na kama ni taasisi ya serikali, toa rufaa ya kesi kwa afisa ustawi wa jamii kwa ajili ya hatua zitakazofuata.

KIAMBATANISHO CHA 5: FOMU YA RUHUSA YA KUONDOKA KATIKA MAKAZI

(tafadhali jaza nakala tatu za fomu hii)

Kuhusu _____ (jina kamili la muathirika),

Ambaye amehifadhiwa _____ (jina la kituo)

Mimi _____ (jina la afisa ustawi wa jamii) natoa ruhusa ya kuondoka kwa muathirika huyu nikiamini kwamba:

A. (Jaza kama inavyostahili) **Ataunganishwa na familia yake au walezi (futa kama inavyostahili)** ☐

Jina: _____

Anuani: _____

Eneo: _____

Namba ya simu: _____

B. Atalelewa na ☐

Jina: _____

Anuani: _____

Eneo: _____

Namba ya simu: _____

C. Anahamishwa kwenda taasisi nyingine ☐

Jina la kituoa cha ulinzi na msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu:

_____

Anuani: _____

Eneo: _____

Namba ya simu: _____

D. Ataunganishwa na jamii yake: ☐

Jina la afisa/ kiongozi wa eneo/kijiji aliyempokea muathirika: _____

_____

Cheo: _____

Anuani: _____Eneo_____

Namba ya simu: _____

Angalizo (*Tafadhali andika taarifa nyingine yoyote ya muhimu kwa ajili ya ufuatiliaji. Kwa mfano: kama muathirika anatumia dawa za matibabu, anahitaji ushauri nasihi na kadhalika.*)

Taarifa za mwenye kituo cha ulinzi na msaada kwa waathirika.

Jina kamili la mwenye kituo: _____

Saini …… Tarehe: ……

Taarifa za afisa anayemsindikiza muathirika:

Jina kamili: ……

Saini: …… Tarehe: ……

Taarifa ya mtu anayempokea muathirika.

Jina kamili: ……

Saini: …… Tarehe: ……

Saini ya afisa ustawi wa jamii: …… Tarehe: ……..

KIAMBATANISHO CHA 6: ORODHA YA NYENZO ZILIZOTUMIKA

1. Mwongozo wa kitaifa wa kuanzisha na Kuendesha Makazi ya Watoto

2. Kanuni za mwaka 2015 za Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu (Namba 27 & 28)

3. Nyenzo ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Shirika la Kimataifa linaloshghulikia masuala ya Wahamaji (International Organization for Migration (IOM): Mwongozo wa jinsi ya kutambua hatari wakati wa kuwasaidia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, fomu ya utambuzi wa familia (eneo) na tathmini ya familia anayotoka muathirika, fomu ya kukubali kurudishwa kwa hiari na ruhusa ya kuchukua taarifa binafsi.

IOM Tanzania

Slipway Road, Off Chole Road
Plot No. 1365, Msasani Peninsula

P.O.Box 9270, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 260 2913/ 260 2935
Email: iomdar@iom.int

www.tanzania.iom.int